TANGAZO LA SERIKALI Na. 429 la tarehe 30/6/2023

# SHERIA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA,
(SURA YA 272)

---

# KANUNI

---

*(Zimetayarishwa chini ya kifungu cha 29(1)(m))*

KANUNI ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA ZA HUDUMA ZA GARI LA MAJI ZA MWAKA 2023

## MPANGILIO WA KANUNI

| *Kanuni* | *Maelezo* |
| --- | --- |
| | SEHEMU YA KWANZA<br>MASHARTI YA UTANGULIZI |
| 1. | Jina. |
| 2. | Matumizi. |
| 3. | Tafsiri. |
| | SEHEMU YA PILI<br>UTARATIBU WA KUSAJILI NA KUFUTA USAJILI |
| 4. | Masharti ya usajili. |
| 5. | Kuepuka migongano kimaslahi. |
| 6. | Kufuta usajili. |
| 7. | Kuhamisha cheti cha usajili. |
| | SEHEMU YA TATU<br>MAJUKUMU YA PANDE ZINAZOHUSIKA |
| 8. | Majukumu ya mtoa huduma. |
| 9. | Majukumu ya Mwenye Leseni. |

## SEHEMU YA NNE BEI

10. Utaratibu wa kuomba bei.
11. Rufaa.

## SEHEMU YA TANO
### MASHARTI YA JUMLA

12. Ukaguzi
13. Makosa
14. Masharti ya Mpito
15. Adhabu ya Jumla
16. Mamlaka ya Udhibiti kuwa na uwezo wa kuongeza taratibu

---

MAJEDWALI

---

SHERIA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA,

(SURA YA 272)

---

# KANUNI

---

*(Zimetayarishwa chini ya kifungu cha 29(1)(m))*

KANUNI ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA ZA HUDUMA ZA GARI LA MAJI ZA MWAKA, 2023

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Maji na Usafi wa Mazingira za Huduma za Gari la Maji za mwaka 2023.

Matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika kusimamia uendeshaji wa gari za maji katika eneo alilopewa Mwenye Leseni.

Tafsiri
Sura ya 272

3. Katika kanuni hizi isipokuwa pale muktadha utakapohitajil vinginevyo:

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira;

"Sheria husika" ina maana ya Sheria Mama yeyote, Sheria, kanuni, agizo, sheria ndogo au sheria yeyote ambayo inahusika na kanuni inayosimamia huduma za magari ya maji

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji iliyoanzishwa chini ya Sheria ya EWURA;

"Bei kikomo" maana yake ni bei ya juu ya mwisho kwa mita ya ujazo moja ya maji atakayotoza mtoa huduma kwa mteja kama ilivyoidhinishwa na EWURA;

Sura ya 414

"cheti cha usajili" maana yake ni cheti kinachotolewa na Mwenye Leseni kwa mtoa huduma kama kilivyoainishwa kwenye Jedwali la Pili;

"mteja" maana yake ni mtu yeyote ambaye anapata huduma

ya maji kutoka kwa mwendeshaji wa gari la maji;

Sura ya 414

"Sheria ya EWURA" maana yake ni Sheria ya Udhibiti wa Nishati na Maji;

"sehemu ya kujazia maji" maana yake ni mahali palipo chaguliwa au kuidhinishwa na Mwenye Leseni patakapotumiwa na mtoa huduma kuchota maji;

"kitu hatarishi" maana yake ni kitu chochote ambacho kitaleta madhara kwenye ubora wa maji;

"mkaguzi" maana yake ni afisa wa Mwenye Leseni au mtu mwingine yeyote mwenye mamlaka ya ukaguzi;

"Mwenye Leseni" maana yake ni Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira yenye leseni ya Mamlaka ya Udhibiti;

"Wizara" maana yake ni Wizara inayoshughulika na huduma ya maji na usafi wa mazingira;

"mtoa huduma" maana yake ni mtu yeyote anayetoa huduma ya maji kwa wateja kwa kutumia gari la maji;

"Bei ya kununulia" maana yake ni bei anayotoza Mwenye Leseni kwa mwendeshaji wa gari la maji kwa kununua maji kutoka mahali pa kuchotea maji;

"Bei" maana yake ni tozo, ada, kiwango cha fedha kinachotozwa kwa kutoa huduma ya gari la maji kama itakavyoidhinishwa na Mamlaka ya Udhibiti.

Sura ya 285

"Baraza" maana yake ni Baraza la Ushindani lililoanzishwa chini ya Sheria ya Ushindani;

"gari la maji" maana yake ni Motokaa au baiskeli inayobeba au inayovishwa chombo chenye ujazo wa lita 200, ikiwa na vifaa kama bomba la maji, pampu ya maji, dira ya maji, ambayo imesajiliwa kwa madhumuni ya kusafirisha, kusambaza, kugawa au kuuza maji safi na salama katika eneo lenye leseni; na

"huduma za gari la maji" maana yake ni utoaji wa huduma ya maji kwa mteja kwa kutumia gari la maji.

## SEHEMU YA PILI
### TARATIBU ZA USAJILI NA KUFUTA USAJILI

Masharti ya Usajili

4.– (1) Mtu hataruhusiwa kutoa huduma ya maji katika eneo lenye leseni kwa kutumia gari la maji isipokuwa pale ambapo gari hilo limesajiliwa na mwenye leseni kwa mujibu wa na Kanuni hizi.

(2) Bila kuathiri matakwa ya kanuni ndogo (1), mtoa huduma aliyekuwepo kabla ya kuanza kutumika kwa Kanuni hizi, ndani ya kipindi cha miezi kumi na mbili baada ya Kanuni hizi kuanza kutumika, atatuma maombi kwa mwenye leseni wa eneo, kusajili kila gari la maji kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hizi.

(3) Maombi yoyote kwa ajili ya usajili yanayofanywa chini ya kanuni ndogo (1) na (2) yatakuwa katika mfumo ulioainishwa kwenye Jedwali la Kwanza na yatajumuisha:

(a) jina kamili la mwombaji, anuani ya biashara, namba za simu, barua pepe na tovuti kama ipo;

(b) nakala halisi ya kadi ya usajili wa gari la maji ikiwa na maelezo ya aina ya gari, namba ya usajili, ujazo na namba ya chesisi;

(c) kama si mmiliki wa gari, kuwepo na mkataba wa ukodishaji gari la maji;

(d) malipo ya gharama za usajili (yasiyorudishika) kama zilivyoainishwa na mwenye leseni ambazo hazitazidi shilingi za kitanzania laki mbili kwa kila gari la maji.

(4) Mwenye leseni, baada ya kupokea maombi chini ya kanuni ndogo (3) na kujiridhisha na usahihi wa maombi, atatathimini maombi hayo kwa kuzingatia mambo yafuatayo;

(a) iwapo maombi yanakidhi matakwa ya sheria husika;

(b) rekodi za utendaji kazi za mwombaji; na

(c) iwapo gari la maji linakidhi matakwa ya kifundi kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Tatu.

(5) Mwenye leseni baada ya kukamilisha tathimini yake chini ya kanuni ndogo (4), ataidhinisha au atarejesha maombi kwa rejea zaidi au kukataa maombi.

(6) Mwenye leseni-

(a) endapo amekubali maombi atatoa cheti cha usajili kama kilivyoanishwa katika Jedwali la Pili; na

(b) Pale ambapo amerejesha maombi kwa marejeo au kukataa maombi, atamjulisha mwombaji kwa maandishi ikiwa ni pamoja na kumpa sababu za kurejesha au kukataa maombi.

(6) Pale ambapo Mwombaji hataridhika na maamuzi ya mwenye leseni, chini ya kanuni ndogi (6) anaweza

kuwasilisha malalamiko yake kwa Mamlaka ya Udhibiti kwa uamuzi zaidi

(7) Mtoa huduma baada ya ombi lake kukubaliwa na kupewa cheti cha usajili na Mamlaka husika chini ya kanuni ndogo (6) ataweza kutambulika kama wakala wa mwenye leseni;

(7) Mtoa huduma wakati wote atawajibika kuzingatia matakwa yote yaliyoainishwa kwenye cheti cha usajili.

(8) Kipindi cha usajili kilichoainishwa kwenye kanuni ndogo (6), kitakuwa miaka mitatu na kinaweza kuongezwa kwa kipindi kingine cha miaka mitatu endapo mtoa huduma ataomba.

(9) Mtu yeyote atakaye kiuka masharti ya kanuni ndogo (1) na (2) atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atatakiwa kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na elfu hamsini au kifungo kisichopungua miezi miwili au adhabu zote mbili.

Kuepuka migongano kimaslahi

5. -(1) Hakuna mwajiriwa wa mwenye leseni atakayeruhusiwa kutoa huduma ya gari la maji.

(2) Sheria yeyote inayosemekana kumpa mamlaka mwajiriwa wa mwenye leseni uwezo wa kusajiliwa, itakuwa batili na haitakuwa na nguvu.

(2) Mtu yeyote ambaye atakiuka matakwa ya kanuni ndogo (1) atakuwa anatenda kosa na akitiwa hatiani atatakiwa kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na elfu hamsini au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili au adhabu zote mbili.

(3) Kwa kanuni hii neno “mwajiriwa” maana yake ni mtu yeyote anayefanya kazi katika ofisi za mwenye leseni au mjumbe wa bodi ya wakurugenzi anayetumikia kipindi chake kwa wakati huo.

Ufutaji wa Usajili

6.– (1) Mwenye leseni anaweza kufuta usajili wa gari la maji iwapo atagundua kuwa;

(a) mtoa huduma anatumia gari la maji kwa shughuli nyingine zaidi ya ile iliyosajiliwa kufanywa;
(b) mwombaji ametoa taarifa za uongo au zisizo sahihi kuhusiana na uendeshaji wa gari la maji;
(c) mtoa huduma anachukua maji kutoka mahali

pasipo husika au mahali ambapo mwenye leseni hajaidhinisha;

(d) mtoa huduma anauza maji kwa bei za juu zaidi kuliko bei kikomo;

(e) mtoa huduma anadanganya kuhusu kiasi cha maji anachouza; au

(f) mtoa huduma ameshindwa kutekeleza majukumu yake chini ya kanuni hizi.

(2) Mtoa huduma ambaye gari lake limefutiwa usajili chini ya kanuni hii ataacha mara moja kutoa huduma na anatakiwa kurudisha cheti cha usajili kwa mwenye leseni.

(3) Mwenye leseni ndani ya siku saba baada ya kufuta usajili wa gari la maji, atamjulisha mtoa huduma kwa maandishi.

(4) Gari la maji lolote ambalo limefutiwa usajili halitakuwa na sifa ya kusajiliwa tena kwa kipindi cha miezi sita baada ya kufutiwa usajili.

Mtoa huduma yeyote ambaye ataendelea kutoa huduma ya maji kwa kutumia gari la maji lililofutiwa usajili chini ya kanuni 6 atakuwa anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kumlipa faini isiyopungua shilingi laki moja na elfu hamsini au kutumikia kifungo kisichozidi miezi sita au adhabu zote mbili.

Kuhamisha cheti cha usajili

7.– (1) Cheti cha usajili kinaweza kuhamishwa kutoka kwa mtoa huduma mmoja kwenda kwa mtoa huduma mwingine

(2) Mtoa huduma ya gari la maji aliyesajiliwa haruhusiwi kuhamisha cheti cha usajili pasipo kwanza kupata idhini ya mwenye leseni.

(3) Maombi ya kuhamisha cheti cha usajili yatafanywa na mhamishaji kwa kuwasilisha taarifa zilizoainishwa chini ya kanuni ya 4(3).

## SEHEMU YA TATU
### MAJUKUMU YA PANDE ZINAZOHUSIKA

Majukumu ya Mtoa Huduma

8. Mtoa huduma kwa wakati wote wa uhalali wa cheti cha usajili atafanya yafuatayo:

(a) kuchota maji kutoka sehemu iliyotengwa au

chanzo kingine cha maji kilichoidhinishwa na mwenye leseni

(b) kusafirisha, kusambaza au kugawa maji safi na salama kwa mteja ambayo yanakidhi viwango vya ubora wa maji ya kunywa;

(c) kuhakikisha kuwa mabomba na vifaa vingine vilivyo fungwa kwenye gari la maji ni salama na vinafanya kazi ili kuzuia uchafuzi wa maji wakati wa kuyasambaza kwa wateja;

(d) kutoa ushirikiano na msaada kwa mkaguzi ili kufanikisha kazi ya ukaguzi wa gari la maji;

(e) Kuweka taarifa za uendeshaji wa gari la maji kwenye kitabu cha kumbukumbu, ikiwa ni pamoja na kiasi cha maji kinachouzwa, vyanzo vya maji na tarehe za kufanya usafi wa gari la maji kwa kutumia kemikali husika, na kuhifadhi kitabu hicho ndani ya gari la maji;

(f) kuweka takwimu za gharama za uwekezaji na uendeshaji;

(g) kuonesha nakala iliyoidhinishwa ya cheti cha usajili, na kuweka bango linaloonyesha bei kikomo ya maji sehemu wazi kwenye gari la maji;

(h) kusafisha kwa kutumia dawa ya kuulia wadudu gari la maji na vifaa vyake kila baada ya miezi sita au wakati wowote inapobainika kuwa uchafuzi wa gari la maji umetokea, na baada ya kusafisha gari la maji kupata cheti cha usafi kutoka kwa mwenye leseni;

(i) kusafisha kwa kemikali ya kuulia wadudu gari la maji na vifaa vyake baada ya kubaini kuwa gari la maji halikuwa linatumika kwa zaidi ya siku thelathini;

(j) kuhakikisha kuwa wakati wote gari la maji linakidhi mahitaji yote ya kitaalam kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Tatu;

(k) kuhakikisha kuwa gari la maji limepakwa rangi husika, lina namba ya usajili kutoka kwa mwenye leseni, maneno “REGISTERED CLEAN WATER TANKER” au “GARI LA MAJI SAFI LILILOSAJILIWA” na alama nyingine yeyote

inayotakiwa na mwenye leseni, vyote hivi viwe vimeandikwa kwa uwazi pande zote za gari ya maji;

(l) kuhakikisha kuwa mabomba yanayotumika na magari ya maji yameandikwa maneno "Maji Safi"; na

(m) kuzingatia matakwa ya sheria husika ikiwa ni pamoja na vigezo na viwango stahiki.

Majukumu ya mwenye leseni

9. (1) Mwenye leseni atahakikisha kuwa wakati wote wa uhai wa cheti cha usajili, mtoa huduma atatekeleza majukumu yake chini ya kanuni hizi

(2) Bila ya kujali masharti ya jumla ya kanuni ndogo (1), mwenye leseni atafanya yafuatayo:

(a) kuchagua, kuendesha na kuendeleza idadi ya kutosha ya sehemu za kuchotea maji ambazo zinafikika kwa urahisi na zenye maeneo ya kutosha ya kuegesha magari ya maji

(b) kuidhinisha matumizi ya maeneo mengine ya kuchotea maji yanayomilikiwa na watu wengine;

(c) kufuatilia ubora na kiasi cha maji kinachosambazwa na watoa huduma;

(d) kuteua maeneo yatakayotumika katika kusafishia magari ya maji na kuandaa utaratibu wa utekelezaji wake;

(e) kuwasilisha kwa Mamlaka ya Udhibiti ripoti ya kila mwaka ya maendeleo ya huduma za magari ya maji;

(f) kuchagua namba ya usajili, rangi kwa ajili ya magari ya maji na alama nyingine inayotambulisha magari ya maji;

(g) kuhakikisha kuwa gari la maji lina maneno "REGISTERED CLEAN WATER TANKER" au "GARI LA MAJI SAFI LILILOSAJILIWA" yameandikwa pande zote mbili za gari la maji na yanasomeka;

(h) kuthibitisha na hakikisha kuwa ujazo wa gari la maji umeandikwa pande zote mbili za tangi na unasomeka vizuri;

(i) kuhakikisha kuwa bei kikomo inayotumika

imeandikwa pande zote za gari ya maji na inasomeka;

(j) kuhakikisha kuwa namba ya simu inayotumiwa na wateja kuwasilisha malalamiko kuhusu huduma imeandikwa pande zote za gari ya maji na inasomeka;

(k) kufuatilia bei ya maji yanayopelekwa kwa mteja na mtoa huduma; na

(l) kwa kila mwaka kutoa taarifa kwenye magazeti ya Kiswahili na kiingereza yanayosambazwa sana, orodha ya watoa huduma pamoja na namba zao za simu, anuani zao za biashara na mahali walipo.

SEHEMU YA NNE
BEI ZA MAJI

Utaratibu wa kuomba Bei

10.- (1) Mwenye leseni anaweza yeye mwenyewe au baada ya kupokea maombi kutoka kwa mtoa huduma, kuwasilisha maombi ya bei ya maji kwa Mamlaka ya udhibiti kama inavyoelekezwa kwenye kanuni za EWURA (Kanuni za Kukokotoa Maombi ya Bei za Maji).

(2) Bila kujali uwepo wa kanuni ndogo (1), mwenye leseni, angalau mara moja baada ya miaka mitatu anaweza kuwasilisha maombi ya kuomba bei ya maji kwa magari ya maji.

(3) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo (2), mwenye leseni anaweza kuwasilisha maombi ya bei ya maji kwa Mamlaka ya Udhibiti wakati wowote itakapogundulika kuwa kuna mabadiliko makubwa katika mazingira ya uendeshaji.

(4) Kwa kuzingatia kanuni ndogo (1), mwenye leseni atawajibika kuitisha Mkutano wa mashauriano na watoa huduma na wateja wao kabla ya kuwasilisha maombi ya mapendekezo ya bei kwa Mamlaka ya Udhibiti.

(5) Bila kujali masharti ya ujumla ya kanuni ndogo (1), maombi ya bei yataambatanishwa na-

(a) barua kutoka kwa Waziri anayehusika na masuala ya maji kuthibitisha uhalali wa maombi ya bei ya maji chini ya kanuni ndogo (1);

(b) maombi ya bei ya maji yanayoelezea

mapendekezo ya bei ya ununuzi na bei ya mwisho kwa mteja;

(c) uthibitisho kwa maandishi kuhusu bei zinazopendekezwa na tarehe ya kuanza kutumika;

(d) kumbukumbu za mkutano zikiambatana na sahihi za wale waliohudhuria mkutano wa mashauriano kama inavyotakiwa chini ya kanuni ndogo (4);

(e) maelezo ya kina ya jinsi mapendekezo ya bei yalivyofikiwa yakiwa katika mfumo wa "Microsoft na Excel"; na

(f) Maelezo ya kina ya faida ambazo wateja watapata kutokana na bei zinazopendekezwa.

(6) Mamlaka ya Udhibiti baada ya kupokea maombi chini ya kanuni ndogo (5), itatathimini maombi hayo ili kujiridhisha na usahihi wa maombi, na baada ya hapo itafanya uchunguzi kulingana na kifungu cha 19 cha Sheria ya EWURA

(7) Baada ya kukamilisha uchunguzi wake Mamlaka ya Udhibiti itaweka bei kikomo za ununuzi na za mteja, na kuzitangaza kwenye Gazeti la Serikali

(8) Mtoa huduma yeyote atakayeuza maji juu ya bei kikomo, anatenda kosa na ukitiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na elfu hamsini au kifungo kisichopungua miezi miwili au adhabu zote mbili.

Rufaa

Cap.285

11. Mtu yeyote ambaye hataridhishwa na uamuzi wa Mamlaka ya Udhibiti, chini ya kanuni 9(7) anaweza kukata rufaa kwenye Baraza chini ya Sheria ya Ushindani.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA JUMLA

Ukaguzi

12. Mkaguzi anaweza kwa kuzingatia maelekezo ya Mwenye Leseni, kukagua gari la maji na taarifa zozote muhimu kwa utoaji wa huduma ya maji, na mtoaji huduma atawajibika kutoa msaada unaotakiwa kuwezesha ukaguzi huo.

(2) Wakati wa ukaguzi, Mkaguzi anaweza -

(a) kutoa nakala za mambo muhimu yanayomsaidia mtoa huduma kutoa huduma ya gari la maji; na

(b) kukagua gari la maji, mashine, vifaa, dira za maji na vifaa vingine vinavyohusiana na utoaji huduma ya gari la maji.

(2) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo (1) Mamlaka ya Udhibiti, wakati wowote ule inaweza kufanya ukaguzi wa gari la maji, na kuomba kupatiwa taarifa muhimu zinazosaidia utoaji wa huduma ya gari la maji na kuchukua hatua stahiki kulingana na matakwa ya Kanuni hizi na sheria husika nyingine.

(3) Endapo uchunguzi wa Mamlaka ya Udhibiti au wa mwenye leseni utabaini kuwa mtoa huduma amekiuka baadhi ya matakwa ya kanuni hizi au sheria husika nyingine, Mwenye Leseni anaweza-

(a) kuchukua hatua stahiki kama zinavyobainishwa katika Kanuni hizi ikiwa ni pamoja na kufuta usajili wa gari la maji; au

(b) kuchukua hatua nyingine kama itakavyoonekana inafaa ili kulinda maslahi ya wateja.

Makosa

13. Mtoa huduma ambaye-

(a) atazuia Mamlaka ya Udhibiti au mkaguzi kufanya kazi zake kama inavyoelezwa katika Kanuni hizi na sheria husika;

(b) anayetukana, anayetishia au kutumia lugha chafu kwa Mkaguzi;

(c) atakataa au atashindwa kutii maagizo halali na maelekezo ya mkaguzi, anatenda kosa, na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na hamsini elfu au kifungo cha miezi miwili au adhabu zote mbili.

Masharti ya Mpito

14. Mtu yeyote anayetoa huduma ya gari la maji ndani ya eneo la Mwenye leseni, katika kipindi cha miezi sita baada ya Kanuni hizi kuanza kutumika, anatakiwa kufanya maboresho katika huduma zake, ikiwa ni pamoja na kupandisha hadhi gari la maji na kufanya ukarabati wa miundombinu husika ili kukidhi matakwa ya Kanuni hizi.

Adhabu ya Jumla

15. – (1) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya Kanuni hizi na hakuna adhabu mahsusi ambayo imetamkwa bayana,

atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na elfu hamsini au kifungo kisichopungua cha miezi miwili au adhabu zote mbili.

(2) Mtu yeyote atakayepatikana na hatia chini ya kanuni ndogo (1) na anaendelea kutenda makosa yaleyale atatakiwa kulipa faini ya shilingi laki moja na hamsini elfu kwa kila siku kwa muda wote kosa linaendelea kutendwa.

Mamlaka ya Udhibiti kuongeza taratibu

16. Pale ambapo hakuna utaratibu uliobainishwa katika Kanuni hizi, Mamlaka ya Udhibiti inaweza kufanya linalowezekana chini ya Sheria, Sheria ya EWURA, na sheria nyingine zinazohusika kuiwezesha kushughulikia suala lolote lililoletwa mbele yake.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetayarishwa chini ya Kanuni 4(3))*

FOMU YA MAOMBI YA KUSAJILI MAGARI YANAYOSAMBAZA MAJI

Malengo ya maombi ni (weka alama "X" katika boksi husika)

(a) Kuomba usajili ☐

(b) Kuomba kuendeleza usajili ☐

(c) Kutoa taarifa ya kubadili umiliki wa gari ☐

(d) Kutoa taarifa ya kusitisha huduma ☐

(e) Kutoa taarifa ya kubadili maelezo ya usajili ☐

SEHEMU YA KWANZA
MAELEZO YA JUMLA

A. Maelezo ya Mwombaji
1. Jina kamili la Mwombaji (waombaji) …………………………………………
2. Anuani ya Mwombaji

S.L.P …………………………….

Nyumba Na. …………. Kiwanja Na. …………… Kitalu Na. …………… Mtaa ……………………….

Jiji / Manispaa / Mji ………………………………………………………………..

Simu Na. ………………………… Simu ya Mkononi Na. ………………………..

Barua pepe ………………………………… Tovuti ………………………………..

B. Hadhi ya kisheria ya Mwombaji (weka alama "X" sehemu husika)

Binafsi ☐ Kampuni ☐ Ubia ☐

Asasi isiyo ya Serikali ☐ Jumuiya ☐

C. Taarifa za Gari la maji

Namba ya usajili wa Gari…………………………………… Ujazo wa tanki ($m^3$)………………………….

SEHEMU YA PILI
SEHEMU HII IJAZWE KWA AJILI YA TAARIFA YA KUBADILI UMILIKI WA GARI TU

Mimi ……………………………………………………………………………… wa S.L.P …………………….. ninatoa taarifa kwamba nimebadili umiliki wa gari kwenda kwa ………………………………………………………………………………………………… …. wa S.L.P …………. kuanzia …………………………….. siku ya …………………….

SEHEMU YA TATU
SEHEMU HII INAHUSU TU TAARIFA YA KUSUDIO LA KUSITISHA HUDUMA

Mimi ……………………………………………………………………………… wa S.L.P …………………………. Ninatoa taarifa kwamba nimesitisha kusambaza huduma ya maji kwa gari katika eneo la ………………………………………………………, kuanzia …………….. siku ya …………… 20…………….

SEHEMU YA NNE

SEHEMU HII IJAZWE KWA AJILI YA TAARIFA YA KUBADILI MAELEZO YA USAJILI TU

Mimi ………………………………………………………………………… wa S.L.P …………………………… Ninatoa taarifa kwamba nimebadili maelezo yangu ya usajili kama ifuatavyo kutoka (jaza maelezo ya sasa ya usajili) ……………………………………………………………………………………… kuwa (jaza maelezo mapya ya usajili) ……………………………………………………………………….

Kuanzia …………………………. Siku ya …………………… 20……………….

SEHEMU YA TANO

NYARAKA ZINAZOWASILISHWA PAMOJA NA FOMU YA MAOMBI

Mambo ya kuangalia (weka alama ya vema sehemu husika)

1. Cheti kilichothibitishwa cha usajili wa gari la maji ☐
2. Ushahidi wa malipo ya ada ya maombi ☐

SEHEMU YA SITA
KIAPO CHA MWOMBAJI (WAOMBAJI)

Mimi / sisi (*futa lisilohusika*), nili/tuliosaini hapa chini, nina/tunakiri kwamba, maombi haya yote, matamko yote yaliyofanyika, viambatanisho vyote na taarifa zote zilizowasilishwa kwa ajili ya maombi haya, kwa utashi wangu/wetu ni kweli, sahihi na kamili kwa vigezo vyote na matakwa yote.

Mimi / sisi (*futa lisilohusika*), nina/tuna elewa kwamba (Weka jina la Mamlaka) wanaweza kufanya uchunguzi kamili wakina kupata usahihi wa maelezo yote yaliyotolewa humu ndani na Mimi/ sisi (*futa lisilohusika*), tunaipa (Weka jina la Mamlaka) mamlaka ya kufanya uchunguzi huo.

Mimi / sisi (*futa lisilohusika*), nina/tunawapa mamlaka wafanyakazi wangu / wetu kutoa maelezo yoyote kama ambavyo kwa sababu zozote yanahitajika na (Weka jina la Mamlaka) kuhusiana na maombi haya.

Mwombaji                                        Shahidi (Kamishna wa Viapo)

Jina kamili ………………………………… Jina Kamili ………………………..

Wadhifa: ……………………………….. Wadhifa: …………………………..

Saini: ……………………………………. Saini na Muhuri …………………

Tarehe: ……………………………………... Tarehe: ………………

---

SEHEMU YA SABA

---

KWA MATUMIZI YA OFISI TU

1. Je Fomu za maombi zimejazwa kwa ukamilifu na kusainiwa na Ofisa aliyethibitishwa na Mwombaji?

Ndio ☐ Hapana ☐

2. Je mwombaji amekidhi matakwa ya usajili wa kutoa huduma ya maji kwa jamii?

Ndio ☐ Hapana ☐

Tarehe ya Kupokea: …………………………... Imepokelewa na: ……………………….

Namba ya Mwombaji: ………………………………………… Saini: …………………………

*Tangazo la Serikali Na. 430 (Linaendelea.)*

KIAMBATISHO CHA PILI

Cheti cha Usajili
(*Imetayarishwa chini ya Kanuni 4(b)(a)*
*(Weka Anuani ya Mwenye leseni)*

Jina la Mwenye Leseni: Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira

CHETI CHA USAJILI WA GARI LA MAJI
(Kimetolewa chini ya Kanuni 4 ya kanuni za maji na usafi wa Mazingira (Huduma za Gari la Maji) 2022

CHETI CHA USAJILI WA GARI LA MAJI Na. …………………………..

Cheti cha usajili wa Gari la Maji kimetolewa kwa ……………………… wa sanduku la posta ………………… kutoa huduma ya Gari la Maji lenye namba za usajili ………………. Kwa masharti ya maelezo yaliyopo kwenye kiambatisho.

Cheti hiki cha usajili kitadumu kuanzia …………. Siku ya …………..,20 ….. na kitaendelea kutumika kwa miezi kumi na mbili (12), isipokuwa kama kitafutwa au kuongezewa muda wake wa kutumika chini ya masharti na maelezo yaliyotolewa kwenye kiambatisho chenye kanuni za Maji na Usafi wa Mazingira (Huduma ya Gari la Maji) 2021.

Mhuri wa Ofisi

…………………………….………

Tarehe ya kutolewa …………………….                                   Mkurugenzi Mwendeshaji

JEDWALI LA TATU

(*Limetayarishwa chini ya Kanuni 4 (4)(c))*

Mahitaji ya Kiufundi ya Gari la Maji

1. Gari la maji liwe na sifa zifuatazo;

(a) Liwe limetengenezwa kutumia malighafi ambazo hazitaathiri usalama wa maji;

(b) Liwe limetengenezwa na kusilibwa kwa kutumia malighafi ambayo ni salama na haitaathiri ubora wa maji;

(c) Liwe katika hali nzuri kiafya na lisiwe na kutu na taka chafu;

(d) Liwe na uwezo wa kustahimili kubabuka;

(e) Liwe imara na kuwa katika hali nzuri kiuendeshaji na lisiwe limegusana na vitu vichafu nahatari;

(f) Kuwe na mfumo unaowezesha unyonyaji au utoaji wa maji yote kwenye tangi la maji na kuwe na sehemu wazi yakutosha ili kuruhusu ukaguzi na usafishaji wa tangi la maji;

(g) Litumike kwa kazi ya kusafirisha na kugawa maji ya kunywa.

2. Gari la maji halitakuwa na sehemu ambazo zitaruhusu maji kutuama na hivyo kuruhusu uwepo wa bakteria.

…………………………………… ……………………………………….

………………….., 2023 Mkurugenzi Mkuu

JEDWALI LA NNE

*(Limetayarishwa chini ya kanuni 8(f)*

UWEKAJI KUMBUKUMBU ZA GHARAMA ZA UWEKEAJI NA UENDESHAJ WA GARI LA MAJI

Namba ya usajili wa Gari la Maji: …………………………………………………. Tarehe ya gari kununuliwa: …………………………………

Uwezo wa tanki la maji (Lita za ujazo) …………………………………………… Eneo: …………………………………………………..

| | Maelezo | Kipimo | Jan | Feb | Mac | Apr | Mei | Jun | Jul | Aug | Sept | Okt | Nov | Dis |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Gharama za Uwekeza ji | | | | | | | | | | | | | |
| 1.2 | Gharama za kununulia Gari la Maji | Shilingi | | | | | | | | | | | | |
| 2 | Gharama zisizobadilika | Shilingi | | | | | | | | | | | | |
| 2.1 | Ada za Leseni | Shilingi | | | | | | | | | | | | |
| 2.2 | Kodi | Shilingi | | | | | | | | | | | | |
| 2.3 | Bima | Shilingi | | | | | | | | | | | | |
| 2.4 | Gharama za Uchakavu | Shilingi | | | | | | | | | | | | |
| 3 | Gharama zinazobadilika kidogo | | | | | | | | | | | | | |
| 3.1 | Gharama za matengenezo makubwa | Shilingi | | | | | | | | | | | | |
| 4 | Gharama zinazobadilika | | | | | | | | | | | | | |
| 4.1 | Posho na mshahara za Dereva | Shilingi | | | | | | | | | | | | |
| 4.2 | Posho na mshahara wa Msaidizi wa Dereva | Shilingi | | | | | | | | | | | | |
| 4.3 | Gharama za mafuta | Shilingi | | | | | | | | | | | | |
| 4.4 | Gharama zakubadilisha matairi na kufanya matengenezo | Shilingi | | | | | | | | | | | | |
| 4.5 | Gharama za | Shilingi | | | | | | | | | | | | |

| | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | kusafisha na dawa ya kuua wadudu | | | | | | | | | | | | | | |
| 4.6 | Gharama za matengenezo ya kawaida | Shilingi | | | | | | | | | | | | | |
| 4.6.1 | Kubadilisha chujio la mafuta | Shilingi | | | | | | | | | | | | | |
| 4.6.2 | Kusafisha Gari la Maji | Shilingi | | | | | | | | | | | | | |
| 4.6.3 | Weka gharama nyingine | Shilingi | | | | | | | | | | | | | |

Dodoma, JAMES A. MWAINYEKULE,

*……………, 2023* *Mkurugenzi Mkuu*